JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI KIFARU

SHULE YA SEKONDARI KIFARU

S. L. P 163

MWANGA.

KUMB.NA KHS/VOL.III/ FOEF/2020

NAMBA ZA SIMU

MKUU WA SHULE 0755- 379021

MAKAMU MKUU WA SHULE 0766 – 480744

MATRON 0672437925

PATRON 0717- 411041

MZAZI/ MLEZI WA WANAFUNZI

……

S. L. P. ……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIFARU HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021/2022

1. Utangulizi

1. **Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiungana kidato cha tano katika shule hii mwaka 2021 tahasusi ya …….**
2. **Shule hii iko kilometa $1^1/_2$ kusini mwa barabara kuu ya Moshi – Dar es salaam unaweza kushukia kwenye kibao cha Shule ya Sekondari Kifaru au Stendi ya mabasi Kifaru.**
3. **Kuanza kwa mihula ya shule itategemea tangazo la serekali.**

2. Mambo muhimu ya kuzingatia :

2.1. Sare ya shule

a) Sare ya shule hii ni sketi mbili kwa wasichana na suruali mbili kwa wavulana rangi ya kijivu) mshono kwa sketi rinda box isiwe ya kubana na ndefu (inch 7 chini ya goti) na suruali iwe na marinda mawili mbele na chini isipungue upana inch 16.

b) Rangi ya hijabu (kijuba) ifanane na shati ya shule (nyeupe) na iwe ndefu yenye kufunika mikono.

c) Sare za michezo ni bukta ya blue, tisheti ya blue isiwe na maandishi na track suti ya blue moja kwa kila mwanafunzi .

d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga kwa kamba venye kisigino vifupi .

e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi

f) Soksi ndefu jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

g) Sweta liendane na rangi ya sare ya shule.

h) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi au nusu kanzu kwa wasichana waislam na iwe ndefu karibia magoti na isiweyakubana.

i) Nguo za kushindia sketi nyeusi kwa wasichana au suruali nyeusi kwa wavulana mshono uwe sawa na sare ya shule na T shirt ya bluu isiyo na maandishi yenye kola(form six)

.

NB: Kwa mzazi /mlezi atakayeshindwa kupata kitambaa stahiki, aje shuleni ataelekezwa kwa fundi kinakopatikana.

2.2. Ada na michango ya shule .

a) Ada ya shule kwa mwaka ni sh 70,000/= unaweza kulipa sh 35,000 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja . fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba 40201100020 benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi na kidato chake kwenye bank pay in slip).

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni :-

i) Sh 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani .

ii) Sh 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha .

iii) Sh 20,000/= kwa ajili ya taaluma.

iv) Sh 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

v) Sh 2,000/= nembo ya shule.

vi) Sh 10,000/= ya huduma ya afya(5,000/= huduma ya kwanza na 5,000/= bima ya afya

vii) Sh 20,000/= mitihani ya kujipima mock .

viii) Fedha ya tahadhari sh 5,000/= (haitarejeshwa)

NB: Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule 40201100020 NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi na kidato chake kwenye pay in slip).

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni :-

i) Ream moja ya karatasi ya photocopy (kwa mwaka)

ii) Vitabu vya masomo kulingana na tahasusi.

a) Daftari 8 kubwa , kalamu ya bluu au nyeusi , pensili na rula.

b) Cofa/ kebe (Mathematical Instruments set).

c) Four figure table (Logarithm table) kwa wanaosoma hesabu.

d) English dictionary (Kamusi ya Kiingereza) na vitabu vingine vya kiingereza (kwa wanaosoma kiingereza).

e) Kamusi ya Kiswahili na vitabu vya Kiswahili (kwa wanaosoma Kiswahili)

f) **Vitabu vya Geography (kwa wanaosoma Geography)**

g) **Vitabu vya History (kwa wanaosoma History)**

h) **Vitabu vya Economics (kwa wanaosoma Economics)**

i) **Vitabu vya Bam (kwa wanaosoma Bam)**

j) **Vitabu vya Advanced mathematics (kwa wanasoma EGM)**

k) **Calculator (Non programmable)**

iii) **Godoro la futi 2.5 aje nalo /yanapatikana kwenye maduka yaliyo jirani na shule**

iv) **Mashuka pea mbili ya kijani , blanket kijivu foronya moja na chandarua kimoja**

v) **Vyombo vya chakula sahani, kikombe kijiko na bakuli**

vi) **Ndoo mbili ndogo zenye mfuniko**

vii) **Vifaa vya usafi na kazi**

<u>Wasichana</u>.

a) **Fyekeo**
b) **Fagio la chelewa refu lenye mpini**
c) **Squezer(mopper)**

<u>Wavulana</u>

a) **Fagio la chelewa refu lenye mpini**
b) **Panga**
c) **Squezer(mopper)**

3. Maagizo

i) **Kila mwanafunzi lazima asome sheria , kanuni na taratibu za shule kwa uangalifu azifuate na kuzitii . Kutofanya hivyo ni makosa.**

ii) **Uvunjaji wa sheria yoyote ya shule hata ikiwa ndogo kiasi gani hautavumiliwa**

iii) **Mwanafunzi lazima ahudhurie vipindi vyote na afanye mazoezi na mitihani ya masomo yote yanayofundishwa darasani kwake. Ni kosa linaloweza kumfukuzisha mwanafunzi shuleni kwa kuacha kuhudhuria vipindi na kuacha kufanya mazoezi / mitihani bila sababu za msingi.**

3.1. <u>Sheria za bweni</u>

i) **Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuchemsha/ kupika bwenini aidha kwa kutumia moto wa kuni, mkaa , mafuta ya taa au moto wa umeme.**

ii) **Bwenini ni mahali pa kulala si pa kupiga kelele. Usemi wa bwenini uwe mazungumzo ya maana ya sauti ndogo . Upigaji kelele au mayowe ni dalili za ulevi , uhuni, fujo, n.k. hiyo haikubaliki.**

iii) **Usafi wa bweni ndani na nje (mazingira yanayozunguka bweni ni wajibu wa kila mkaaji wa bweni husika)**

iv) **Ni makosa kukaribisha mgeni wa aina yoyote bwenini au katika eneo la bweni**

v) **Vyoo vyote lazima vitumike vizuri na kuwekwa katika hali ya usafi**

vi) **Ni wajibu wa viongozi wa bweni pamoja na wana – bweni wote kulinda sheria kwa kuzitekeleza kwa vitendo.**

vii) **Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na vyombo vifuatavyo:- Redio , pasi, Heater, Kamera . Simu ya mkononi, kitu chochote kinachohusiana na simu , Hot pot, Walk man au kifaa chochote cha muziki , Sufuria , Pombe , Madawa ya kulevya , manukato (perfume).**

NB: Mwanafunzi atakayekutwa na vitu tajwa hapo juu atachukuliwa hatua kali. Unaweza kuja na chupa ndogo ya chai (Thermos)

3.2.<u>Makosa yanayoweza kusababisha mwanafunzikufukuzwa shule mara moja ni</u>

1. **Wizi**
2. **Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro**
3. **Kugoma na kuhamasisha mgomo .**
4. **Kutoalugha chafu kwa wanafunzi wenzake , walimu/ walezi na jamii kwa ujumla.**
5. **Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote.**
6. **Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo uliokubalika na shule (Shule yetu hairuhusu kusuka).**
7. **Kufuga ndevu**
8. **Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya**
9. **Uvutaji wa sigara**
10. **Uasherati , uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.**
11. **Kupata ujauzito/ kutoa mimba .**
12. **Kushiriki matendo ya uhalifu , siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.**
13. **Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana .**
14. **Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.**
15. **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi,au kuwa na kifaa chochote kinachohusiana na simu katika mazingira ya shule.**
16. **Kudharau bendera ya Taifa .**
17. **Kufanya jaribio lolote la kujiua , au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k**
18. **Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi**

4. Viambatisho na fomu muhimu

i) Fomu ya mapokezi na utambulisho

ii) Fomu ya uchunguziwa afya (Medical examination form) isainiwe na daktari wa Wilaya.

iii) Hati ya utii na sheria.

iv) Fomu maalum ya wageni ziambatane na picha nne za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kutembelea shuleni na namba zao za simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KIFARU SEKONDARI

Saini ya Mkuu wa Shule ……

Jina la Mkuu wa Shule……..

Mhuri wa Mkuu wa Shule……..

FOMU YA MAPOKEZI SHULENI
MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI (IRUDISHWE SHULENI)

SEHEMU: "A" – Ijazwe na mwanafunzi;

Jina la Mwanafunzi (majina matatu)

……

Anwani; ……..

Taifa / Uraia : ……..

Dini : ……..

Tarehe ya kuzaliwa :……. Jinsia :……..

Shule anakotoka (Shule ya Sekondari) :…… ……..Kata ya …….

Mwaka wa kumaliza kidato cha nne : ……..

Wilaya anakotoka :…….

Mkoa :……..

SEHEMU "B" (Ijazwe na mzazi/ mlezi)

Jina la mzazi / mlezi (majina matatu)

…….

Anwani ya mzazi/ mlezi :…….

Namba ya simu ya simu ya mzazi / mlezi……

Mahali anapoishi : ……

Kazi ya mzazi / mlezi……

Mahali anapofanya kazi : …….

SEHEMU "C"

d) **Tafadhali fika na vifaa vyote ulivyoagizwa**
e) **Wahi shuleni kabla ya saa 11:00 jioni**
f) **Mzazi hakikisha unakamilisha malipo yote kabla ya kumleta mwanao shuleni .**

……..
SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI

…….
SAHIHI MKUU WA SHULE

FOMU MAALUM KWA AJILI YA WAGENI WA WANAFUNZI HAPA SHULENI (IRUDISHWE SHULENI)

FORM NA. KHS/1/2020

A. NDUGU MZAZI.

Kwa kuwa Mwanafunzi amekabidhiwa kwa walezi ambao ni walimu pamoja na wafanyakazi wa shule hii, tunaomba utuorodheshee majina ya jamaa wa karibu watatu tu ambao unaweza kuwatuma kuja kumwona kwa sababu maalum tu.

NA.	JINA	UHUSIANO	KAZI YAKE	MAHALI ATOKAPO	NA. YA SIMU
1					
2					
3					

Mtu mwingine zaidi ya hao waliotajwa hapo juu haruhusiwi / mpaka alete barua ya kumtambulisha .

Mzazi/ mgeni yeyote akija aonane kwanza na uongozi wa shule (Mwalimu wa zamu au mlinzi) na ndio watakaomwita mwanafunzi.

N.B. Mwanao akikutwa / akitoroka kwenda kwenye sehemu za starehe muda wowote atakuwa amejifukuza shule mwenyewe moja kwa moja

Kama mwanao atarudi nyumbani wakati usio wa likizo atakuonyesha kibali maalum cha kutoka shuleni chenye muhuri husika wa shule , utapewa usaini kabla ya kukirudisha.

B. Siku za kuwatembelea wanafunzi rasmi ni jumamosi na jumapili ya Mwisho au mwanzo wa kila mwezi.

C. Mimi mzazi wa …….. Nakubaliana na yote yaliyoandikwa hapo juu.

Naahidi kushirikiana nanyi.

Nikikiuka taratibu hizo mwanangu achukuliwe hatua kali za kunidhamu.

……
SAHIHI YA MZAZI /MLEZI

…….

SAHIHI MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Shule ya Sekondari Kifaru,
S. L. P. 163,
MWANGA.

Tarehe:…….

HATI YA UTII NA SHERIA

Mimi …….. Mzazi / Mlezi wa …….. nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika Maagizo kwa Wazazi na nazikubali Sheria hizo na nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazizingatia kwa manufaa ya Umma.

Mimi ……(majina matatu ya mwanafunzi) Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali Sheria hizo. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

…… ..... …….....
SAINI YA MWANAFUNZI SAINI YA MZAZI

TAREHE:……

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS

KIFARU SECONDARY SCHOOL.
P. O. BOX 163,
MWANGA.

DATE:……

REF: NO. KHS/MEX/VOL.II/2020

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM.

TO THE MEDICAL OFFICER,
……..
…….
…….

Please examine …… (Name of students) who has been selected to join this school for his fitness as a student in the following (To be completed by a medical officer)

1. **Eye sight ……..**
2. **Hearing…….**
3. **Limbs……**
4. **SPECIMEN**
   - **i) Stool…….**
   - **ii) Urine……**
   - **iii) Blood……**
   - **iv) Neurosis……..**
5. **Asthma…….**
6. **Tuberculosis ……**
7. **Pregnancy ……**
8. **Other serious disease:-**
   - **i) Venereal disease……..**
   - **ii) Leprosy ……..**
   - **iii) Epilepsy ……..**
   - **iv) Ulcers ……**

MEDICAL CERTIFICATE:
(To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above and consider him/ her to be physically fit / unfit as a student .
Date: ……. Signature: ……
Station : ……. Designation:…….
NB: I request this form to be returned to the school in a sealed – envelop.

…….
THE HEADMASTER